


# **Mosi and the lion and The ant and the grasshopper**



**English fables  
English - Swahili Translation  
Translated by Fidelis Phene**

## Mosi and the lion - Mosi na simba

It was a scorching day and the mighty Lion gracefully reclined under the shade of a towering tree. His splendid golden mane glistened in the radiant sunlight, a symbol of his untamed but majestic nature. Nestled among the nearby bushes, Mosi, a tiny mouse with soft grey fur darted to and fro looking for tasty morsels to eat.



Ilikuwa siku ya jua kali na simba hodari akajipumzisha kwa adabu chini ya kivuli cha mti mrefu. Hariri yake ya dhahabu ilionekana ikiangaza katika mwanga mkali wa jua, ishara ya asili yake yenye nguvu lakini ya utukufu. Akiwa amejificha kati ya vichaka vilivyoko karibu, Mosi, panya mdogo mwenye manyoya meupe ya kijivu, alikuwa akiruka hapa na pale akimtafuta chakula kitamu cha kula.


Mosi alimtazama mnyama mwenye nguvu kwa mshangao. Kwa uangalifu, akiwa na viruji vyake vidogo vikining'inia, alimkaribia simba, akiona kwamba mguu wake ulikuwa umenaswa kwenye mzunguko uliopindika wa kamba.

Mosi looked at the mighty beast with awe.

Cautiously, with his little whiskers wiggling, he approached the lion, noticing that his paw was caught in a tangled mess of rope. When the Lion noticed Mosi, he turned his head and looked at the small visitor and acknowledging him with a gentle nod. "Great Lion," Mosi said, speaking softly like a gentle breeze, "I may be small, but I can help you if you give me a chance."

The Lion, interested in what Mosi had to say, let out a deep, rumbling laugh. "Little one, how can you help someone as big as me?"

Mosi's eyes sparkled with determination. "Even though I'm small, I can still help. Someday, you might need me. When that happens, I promise to be there for you."



Simba alipomwona Mosi, aligeuza kichwa chake na kumtazama mgeni mdogo, akimkubali kwa kumpungia kichwa kidogo. "Simba Mkuu," Mosi alisema, akiongea kwa sauti laini kama upepo mwanana, "Ingawa mimi ni mdogo, naweza kukusaidia ikiwa utanipa nafasi." Simba, akiwa na hamu ya kusikia maneno ya Mosi, alitoa kicheko kirefu kilichosikika kama mtetemeko wa ardhi. "Mdogo wangu, unawezaje kunisaidia mimi ambaye ni mkubwa namna hiyo?" Macho ya Mosi yalitamalaki kwa azimio. "Hata ingawa mimi ni mdogo, bado naweza kusaidia. Siku moja, huenda ukahitaji msaada wangu. Wakati huo, nakuahidi kuwa nitakuwepo kwako."



Touched by Mosi's words, the Lion smiled. He lifted one of his powerful paws and gently tapped it on the grass. "If you can free my paw from this trap," the Lion said, "then I'll know your promise is true." There was a pause as if Mosi was hesitating, but feeling brave and determined, Mosi eventually scurried forward.

The Lion looked on as Mosi gnawed at the rope, bit by bit, eventually freeing the Lion's paw.

Kuguswa na maneno ya Mosi, simba alionyesha tabasamu. Alinyoosha moja ya makucha yake yenye nguvu na kwa upole akagonga kwenye nyasi. "Ikiwa unaweza kunifungulia mguu wangu kutoka kwenye mtego huu," simba alisema, "basi nitajua ahadi yako ni ya kweli." Kulikuwa na ukimya kana kwamba Mosi alikuwa anasita, lakini akiwa na ujasiri na azimio, hatimaye Mosi alisogea mbele kwa haraka. Simba alimtazama Mosi akiguguna kamba kidogo kidogo, hatua kwa hatua, hatimaye kumfungulia mguu wa simba.



Feeling very grateful, the Lion was amazed by Mosi's determination. From that day on, the Lion and the mouse became great friends. The Lion used his strength to protect the animals and Mosi, thankful for the Lion's friendship, continued to scurry through the land, spreading stories of how even the smallest friends can make a big difference.


Akijawa na shukrani, simba alishangazwa na azimio la Mosi. Tangu siku hiyo, simba na panya wakawa marafiki wazuri. Simba alitumia nguvu zake kulinda wanyama na Mosi, akishukuru kwa urafiki wa simba, aliendelea kukimbiza katika ardhi, akisambaza hadithi za jinsi hata marafiki wadogo wanaweza kufanya tofauti kubwa.





## The ant and the grasshopper


Once upon a time, in a sunny meadow, there lived an ant and a grasshopper. The ant was a very hardworking little creature, always busy collecting food and preparing for the winter. The grasshopper, on the other hand, loved to sing and play all day long.



Iliyokuwa zamani, katika shamba lenye jua, kulikuwa na sisimizi na panzi. Sisimizi alikuwa kiumbe mdogo mwenye bidii sana, daima akiwa na shughuli ya kukusanya chakula na kujiandaa kwa majira ya baridi. Panzi, kwa upande mwingine, alipenda kuimba na kucheza mchana kutwa.

One warm summer day, as the grasshopper was hopping and chirping happily, it noticed the ant carrying grains and storing them in its tiny home. Curious, the grasshopper curiously asked the ant, "Why are you working so hard, dear ant? Come and enjoy the beautiful day with me!" The ant paused for a moment, looking at the grasshopper kindly. "Oh, dear grasshopper," said the ant, "I am preparing for the winter when food will be scarce. It's important to work now and save for the future."

The grasshopper giggled and replied, "Winter is so far away, my friend! Let's sing and dance together. There's plenty of time to worry about winter."




Siku moja ya joto kali, huku panzi akihoppinga na kupeperusha sauti za furaha, aliona sisimizi akibeba nafaka na kuzihifadhi katika nyumba yake ndogo. Kwa mshangao, panzi akamwuliza sisimizi kwa mshangao, "Kwa nini unafanya kazi kwa bidii sana, ewe sisimizi? Njoo ujifurahishe katika siku nzuri pamoja nami!" Sisimizi akasimama kwa muda, akimtaazama panzi kwa upole. "Oh, ewe panzi mpenzi," sisimizi akasema, "Ninaandaa kwa ajili ya majira ya baridi ambapo chakula kitakuwa adimu."

Ni muhimu kufanya kazi sasa na kuokoa kwa ajili ya siku zijazo." Panzi akacheka kwa furaha na akajibu, "Majira ya baridi yapo mbali sana, rafiki yangu! Tucheze na kuimba pamoja. Kuna muda mrefu wa kuwaza kuhusu majira ya baridi."

As the days turned into weeks and the weeks into months, winter finally arrived. The once-green meadow turned white with snow, and all the food was buried under the cold ground. The grasshopper, now feeling hungry and cold, realised its mistake. It hadn't prepared for the winter like the wise ant did. With a sad face, the grasshopper approached the ant and said, "Dear ant, I was wrong not to listen to you. I have no food or shelter for the winter. Can you help me?"

The ant, remembering its kindness, nodded and said, "I have enough food for both of us. Come and share it with me. But remember, it's important to plan and work for the future."



Siku zilikwenda na kuwa wiki na wiki zikawa miezi, hatimaye majira ya baridi yalifika. Shamba ambalo awali lilikuwa kijani likageuka kuwa jeupe kwa theluji, na chakula chote kikafukiwa chini ya ardhi baridi. Panzi, sasa akiwa na njaa na baridi, aligundua kosa lake. Hakujitayarisha kwa majira ya baridi kama alivyofanya sisimizi mwerevu. Kwa uso uliojaa huzuni, panzi alimwendea sisimizi na kusema, "Ewe sisimizi, nilikuwa na makosa kwa kutokukusikiliza. Sina chakula wala makazi kwa ajili ya majira ya baridi. Je, unaweza kunisaidia?" Sisimizi, akikumbuka wema wake, akakunja kichwa na kusema, "Nina chakula cha kutosha kwa sisi wote. Njoo ujishirikishe nacho. Lakini kumbuka, ni muhimu kupanga na kufanya kazi kwa ajili ya siku zijazo."



From that day on, the grasshopper learned the importance of hard work and preparation. It helped the ant with various tasks, realising that there is a time for play and a time for work. The ant and the grasshopper became good friends, supporting each other in times of need. They danced and sang together during the warm summer days, but when winter approached, they worked side by side, ensuring they were both prepared. The ant and the grasshopper lived happily ever after, teaching us the valuable lesson of balancing work and play and the importance of planning for the future.



Tangu siku hiyo, panzi akajifunza umuhimu wa kazi ngumu na maandalizi. Ilikuwa msaada kwa sisimizi katika majukumu mbalimbali, akigundua kwamba kuna wakati wa kucheza na wakati wa kufanya kazi. Sisimizi na panzi wakawa marafiki wema, wakisaidiana wakati wa mahitaji. Walicheza na kuimba pamoja katika siku za joto zenye joto, lakini wakati majira ya baridi yalipokaribia, waliweka kazi pembeni, wakihakikisha kuwa wote wawili wamejiandaa. Sisimizi na panzi waliishi kwa furaha milele baada ya hapo, wakitufundisha somo muhimu la kudumisha usawa kati ya kazi na mchezo na umuhimu wa kupanga kwa ajili ya siku zijazo.